



CHUO KIKUU CHA NAIROBI

CHUO CHA ELIMU NA MASOMO YA NJE

BEWA LA KIKUYU

IDARA: IDARA YA LUGHA NA FASIHI

KOZI:

KODI: TKS

SWALI:

MHADHIRI: Dkt.

KAZI INAWASILISHWA NA:

NAMBARI YA USAJILI:

SAHIHI: _____

TAREHE YA KUWASILISHA: NOVEMBA 14, 2014.

YALIYOMO

UKURASA

1.0: UTANGULIZI.....1.0

2.0: MAANA YA METHALI.....	2.0
3.0: SIFA ZA METHALI.....	2.0
4.0: DHIMA YA METHALI.....	4.0
5.0: MUUNDO WA METHALI.....	5.0
6.0: HITIMISHO.....	7.0

Utangulizi

Katika kazi hii nitaweza kushughulikia matatizo yanayokumba uainishaji wa lugha nchini Kenya kwa kurejelea wataalamu mbalimbali. Wataalamu hawa ni pamoja na: w.h. whitely,malcom Guthrie, greenberg , lucia omondi na okoth okombo.

Kimsingi lugha za nchini Kenya zinaweza kuainisha kwa kuzingatia makundi mawili muhimu. Makundi haya ni pamoja na:

Lugha asilia

Lugha za kigeni

Makundi haya mawili huweza kushughulikia lugha zote nchini Kenya kiuainishaji. Kenya kama mojawapo wan chi barani afrika, inazo lugha nyingi ukilinganisha na mataifa mengine duniani. Kwa hivyo idadi kamili ya lugha zilizoko nchini Kenya haijulikani kutokana na ukosefu wa

utafiti wa kina kuonyesha lugha ni ipi na lahaja ni ipi?. Kwa hivyo hili ndilo mojawapo ya matatizo ambayo hukumba wataalamu katika harakati zao za uainishaji lugha.

Lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana.

Kuainisha ni kugawa neno katika viambishi vyake mbalimbali. Wakati neon linapoinishwa, mzizi wa neno pamoja na viambishi vyote vilivyofungamanishwa kuunda neno hilo huonyeshwa. Kwa pia katika kuainisha lugha mambo haya huweza kutokea.

Lugha asilia nchini Kenya

Lugha asilia ni lugha ambayo hutokana na jamii mahsusi ambamo imeibuka na kufungamana kiutendajji na katika utamaduni na maendeleo ya jamii husika. Kwa mfano Kiswahili ni lugha asilia ya wakenya katika jamii ya kikenya.

Lugha asilia imeweza kugawika katika makundi matatu muhimu. Makundi haya ni pamoja na:

Lugha za kibantu

Lugha za kinailoti **Lugha za Kinilo-Sahara** ni familia ya lugha barani [Afrika](#). Katika familia hiyo kuna lugha takriban 200 zenye wasemaji milioni 35 katika nchi za [Mali](#), [Niger](#), [Chad](#), [Sudan](#) na Afrika Mashariki, k.m. [Kijaluo](#) na [Kimaasai](#). Matatizo yake wanaozungumza lugha hizi ni wafugaji wa kuhamahama.

Lugha za kikushiti

Lugha za kibantu

Hili ni kundi la lugha ambalo ni tawi la lugha za naija-kongo. Bantu maana yake ni watu katika lugha nyingi za kundi hilo. Wataalamu mbalimbali waliweza kuziainisha lugha za kibantu kama ifuatavyo.

Malcolm Guthrie

Mtaalamu huyu aliweza kuziainisha lugha za kibantu kwa kulinganisha na maeneo ya kijiografia.

Lugha za kiluhya

Mtaalam Guthrie aliweza kuzigawa lugha za kibantu za kiluhya katika makundi yafuatayo:

1. Kibukusu iko katika kundi la E.30, hasa moja ya lugha za Kiluyia.
2. Kikabaras iko katika kundi la E30.
3. Kilogooli iko katika kundi la E40.
4. Kiidakho iko katika kundi la E40.
5. Kisaamia iko katika kundi la J30 (zamani iliitwa E30).
6. Kiidakho iko katika kundi la E40
7. Kiidakho iko katika kundi la E40.
8. Kimarama iko katika kundi la E30.
9. Kinyore iko katika kundi la E30.

Kwa hivyo kutokana na makundi haya ya uainishaji ya mtaalamu Malcolm Guthrie tunaona inaleta matatizo katika uainishaji wa kisasa. Hii ni kwa sababu yeye aliweza tu kuteua baadhi ya lugha na kuzifanyia majaribio bila kuzingatia mpangilio wowote. Guthrie anatia kinyore, kimarama, na kikabras katika kundi moja la E.30 kwa sababu zinazunguzwa katika sehemu ya kijiografia moja. Yaani lugha hizi zote ni lugha za kiluhya. Hali hii imeweza kuleta matatizo chungu nzima kwa sababu makala haya hayawezi kutegemewa, kwa vile lugha zinazoundwa upya na kwa hivyo ukoo unaweza kuwa tofauti iwapo mmoja atabadilisha chaguo la lugha.

Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu ambayo chimbuko lake ni upwa wa Afrika Mashariki. Lugha hii ilianishwa na Guthrie (1948) kama lugha ya Kibantu ya kundi la G. Kiswahili kina lahaja nyingi. Lahaja zilizobainishwa na Guthrie (1948) ni kumi na nane. Lugha hii ni lingua franca na inazungumzwa na watu wengi katika maeneo mengi tofautitofauti ya Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na Kusini. Aidha, inazungumzwa katika eneo la kusini mwa Oman kule Uajemi (Polome, 1967; Mbaabu, 1991; Chimerah, 1998).

Kiswahili ni lugha ya kitaifa na pia lugha rasmi nchini Kenya na Tanzania. Katika sera za lugha za nchi hizi mbili, Kiswahili kimejumuishwa kama somo rasmi katika mitaalaa ya elimu na hivyo kinafundishwa kuanzia shule za msingi, za upili, pamoja na vyuo vikuu. Pia lugha hii hutahiniwa

katika mitihani ya kitaifa katika shule za msingi na za upili katika nchi za Afrika Mashariki. (Iribemwangi na Mukhwana 2011).

Lugha ya Kiswahili inatambuliwa kama lugha ya kimataifa kwa sababu inatumika katika shughuli za kiuchumi, kidini na kisiasa katika ngazi za kimataifa. Vyuho vingi barani Afrika, Ulaya, Asia na Marekani vinafundisha somo la Kiswahili. Vituo vingi vya redio hurusha matangazo yao kwa lugha ya Kiswahili pia.

Kiswahili ni miongoni mwa lugha zilizotafitiwa sana na kuandikiwa vitabu vingi na makamusi. Maandishi mengi ya Kiswahili yamechapishwa na kusambazwa yakiwemo majarida, vitabu vya dini, riwaya, tamthilia, mashairi na nyimbo zinazoimbwa pamoja na vitabu vya hadithi fupi. Kazi nyingi pia zimetafsiriwa kwa Kiswahili. Wazungumzaji wa Kiswahili wanakadiriwa kuwa zaidi ya watu milioni 140, (Chimerah 1998; Lewis na wenzake 2013) katika makala ya Ethnologue Toleo la 17.

Kwa hivyo kutokana na uainisho wa Guthrie wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kibantu anaiweka katika kundi la G. Kwa hivyo yeye aliweza tu kubainisha lahaja za Kiswahili 18 pekee. Jambo hili linakuwa tatizo katika uainishaji wa kisasa.

Lugha ya Ekegusii

Lugha ya Ekegusii, kama lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Lugha hii inazungumzwa katika kaunti za Kisii na Nyamira ambazo ziko kusini magharibi mwa nchi ya Kenya. Miji mikuu ya kaunti hizi ni Kisii na Nyamira mtawalia. Guthrie (1948) amebainisha lugha ya Ekegusii kama lugha ya Kibantu ya kati ambayo iko kundi moja na lugha ya Kikuria katika kundi la E.42. Lugha hii inahusishwa na lugha ya Lagooli, Kikuria na Kimeru za Kenya, Ware, Ikisu, Ikoma na Sanjo zote za Tanzania.

Jamii ya Abagusii imezingirwa na jamii nyingine ambazo si jamii-lugha moja nayo. Upande wa magharibi imepakana na jamii ya Waluo na upande wa kaskazini imepakana na jamii ya Wakipsigis. Imepakana na Wamaasai upande wa kusini. Asili ya Abagusii ni eneo

lililo kati ya Nigeria mashariki na Cameroon. Baadaye walihamia Congo kabla ya kuingia nchini Kenya kutoka upande wa magharibi na kutulia katika milima ya Gusii (Kapiyo na wenzake 1996). Idadi ya Abagusii ni zaidi ya watu milioni 2.2 ambao ni asilimia kumi ya jumla ya watu nchini Kenya kuambatana na takwimu za sensa ya (2009).

Jamii hii ina watu wengi mno mashambani nchini Kenya ikilinganishwa na maeneo mengine. Kuna watu takriban 500 katika kila kilomita mraba. Asilimia kubwa ya Abagusii ni wanauwili-lugha kwa maana kuwa watu wengi wa jamii hii wanazungumza zaidi ya lugha moja. Jamii ya Abagusii wanaipenda na kujivunia lugha yao.

Kutokana na maelezo haya tunaona kuwa Guthrie alikuwa akitegemea kigezo cha kijiografia katika uainishaji wake na hii basi kuwa tatizo katika uainishaji wa lugha.

Lugha za Ekegusii na Kiswahili ni lugha za Kibantu. Lugha za Kibantu ni ambishi. Lugha hizi huambatisha vambishi kwenye mizizi ya maneno ili kuunda maneno mapya. Viambishi hivyo hubeba maana za njeo, idadi, nafsi, hali, kauli, ukanushaji na ngeli (Polome, 1967; Guthrie, 1970; Massamba, 2004). Maneno ya lugha za Kibantu hufuata muundo wa konsonanti, vokali, konsonanti na vokali.

Lugha hizi zina matumizi mengi ya umaanisho katika mazungumzo kwenye miktadha mahususi. Kategoria mahususi za kisemantiki zinapotumiwa katika miktadha fulani kimazungumzo huzua umaanisho. Utatahuwa unazuka iwapo miktadha ya matumizi ya kategoria fulani za kisemantiki haibainiki. Matumizi ya lugha kimazungumzo hubainisha uwazi na umaanisho katika miktadha mbalimbali. Kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano, utafiti huu ulibainisha maana za baadhi ya kategoria za kisemantiki katika lugha ya Ekegusii na kuilinganisha na zile za Kiswahili ili kuonyesha iwapo kuna mshabaha wowote wa matumizi ya kategoria za kisemantiki katika miktadha ya kijamii mnamotumika lugha hizi.

Tofauti moja kubwa inayobainika kati ya lugha za Kiswahili na Ekegusii ni ile ya kisauti ambapo katika lugha ya Ekegusii, sauti ambayo sighthuna huwa ghuna inapofuatwa na sauti nyingine sighthuna kulingana na sheria ya Dahl. Sifa hii hubainika katika lugha za Kibantu za Kaskazini

Mashariki. Sifa hii haibainiki katika lugha ya Kiswahili. (Bickmore, 1998). Katika lugha ya Ekegusii pia toni inaweza kuzua umaanisho kwa vile ina jukumu muhimu sana kama kipengele cha muundo wa lugha hii kinyume na lugha ya Kiswahili.

w. h. whitely

mtaalamu huyu aliweza kuainisha lugha baada ya Guthrie, Brian na Greenberg. Kwa yeye ndiye mtaalamu wa hivi karibuni katika kuainisha lugha za Kenya. Whitely aliweza kutumia kigezo cha kiantropolojia katika uainishaji wake. Kigezo hiki kinakuwa tatizo kuu katika uainishaji lugha kwa sababu kilikuwa kiko nje na kilikuwa kinashughulikia tu mahusiano baina ya lugha na utamaduni.

Whiteley(1974). Anaweka lugha yac lulogoli katika kundi moja na lugha ya Ekegusii au kikisii kwa sababu yeye aliona kwa walogoli walikuwa wameloweza sana katika mji wa kisii na hivyo basi akaainisha lulogoli na Ekegusii katika kundi moja. Mambo haya sivyo jinsi Whiteley alivyoyaaainisha kwa sababu wamaragoli walikuwa wanaishi tu huko kisii ili kujiendeleza kimaisha na hali ya kuongezeka kwa mjini kissi hukuwezi fanya lulogoli iwe katika kundi moja na Ekegusii.

Vilevile Whiteley aliweza kutia lugha ya kipokomo katika lugha za mijikenda katika uainishaji wake. Kwa hivyo hili linakuwa ni tatizo kubwa sana katika uainishaji wa lugha. Kabila za mijikenda ni tisa yaani jina hili lina maana ya makabila tisa na haya ni pamoja na: di hivi tisa ni: Wadigo, Wachonyi, Wakambe, Waduruma, Wakauma, Waribe, Warabai, Wajibana na Wagiriama.

Kwa upande mwingine kipokomo na kipokot zimo katika kundi moja la uainishaji lugha kundi la E. 70. Kwa hivyo hali ya Whiteley kuweka lugha hii katika kundi moja na kundi la mijikenda ni hali potovu.

Vilevile whitely aliweza kutia lugha ambazo haziingiliani kabisa katika kundi moja. Kwa mfano alichukuwa lugha ya lukabras na kuitia katika kundi sawa na lugha ya Ekegusii.

Kwa uainishaji wa whitely unayo matatizo chungu nzima kwa kuwa alikuwa anategemea misingi ambayo iliwekwa mwanzo na wataalamu waliomtangulia.

Mtaalamu okoth okombo kwa upande wake aliweza kuzungumzia hali ya lugha za ishara kupuuzwa.

Mtaalamu lucia omondi naye kwa upande wake alizungumzia lugha nchini Kenya ambapo anasema lugha zinazopatikana katika kaskazini mashariki zina matatizo kuwekwa katika makundi mengine nchini Kenya.

Lugha za kigenik.m kiingereza na kihindi zinatumika katika elimu

Kihindi na kiurdu kinatumika na watu waliokuja kama walowezi wanafanya biashara baada ya ukoloni.

Lugha za bureli ishara hutumiwa katika shughuli rasmi nchini Kenya. Kiuamilifu-kutolea elimu

Kuendesha shughuli za serikali siasa mahakama

Kkufanya mawasiliano ya kawaida miongoni mwa watu

Katika biashara

- ✓ Kile cha kijiografia
- ✓ Kile cha unasaba wa lugha
- ✓ Kile cha uamilifu wa lugha
- ✓ Kile cha umuundo

a) KIGEZO CHA KIJIOGRAFIA

Hutumika kuainishia lugha pale ambapo si mengi yanajulikana kuhusu lugha Fulani husika kutokana na ukweli huu mbinu hii inakuwa ni ya kimsingi Zaidi katika uainishaji lugha japo ni ya kijumla mno na uwa na chukulizi nyingi,kutokana na mbinu hii tunaweza kuzungumzia lugha za afrika zipattikanazo eneo kujulikanao kama afrika au za lugha za upwa wa kenya

b) KIGEZO CHA UNASABA

Kigezo hiki ni cha kisayansi kwa sababu uzingatia unasaba wa lugha uliop kwa kuegemea hasha msamiati wa kimsingi au kilimwengu pamoja na mabadiliko ya kiwakati yanayozipitikia lugha husika mbinu hii ya uainishaji lugha uzingatia muundo wowote wa lugha kutoka kwenye sauti hadi kwenye sentensi na kuweza kubaini kama kweli lugha Fulani ni za ukoo moja au la. Hali hii ndio izarizayo dhana za mame-lugha, binti lugha na dada lugha

Mame-lugha kama dhana ,ni dhana ya kufikirika tu kwa kuwa hapana popote ulimwengu,lugha hii iwezo kupatikana ikitumika katika mawasiliano. Lugha hii ijulikanayo kama mame lugha uwezo kupatikano kutokana na ujengaji upya lugha. Hali hii ya kujenga upya lugha ujidhihirisha pale ambapo lugha mbili au Zaidi uweza kulinganishwa na kulinganuliwa kwenye swala nzima la muundo na kisha kuonyesha ruwaza Fulani katika tofauti za kimuundo zilizopo. Hali iwapo hivi lugha husika usemekana kuwa ni dada lugha kwa kuwa zimetokana na mame-lughamoja. Lugha zizi hizi uwa nib inti-lugha kwa mame-lugha iliyoizaa.

Ni kwa matumizi ya kigezo hiki cha uainishaji lugha ambapo sir William tones alijitokeza na dhana ya lugha za kihindi kizungu ambyo imeziza lugha zipatikanazo bara hindia na bara uropa

Katika kielezo hiki A ndio inayojitokeza kama lugha mzazi kwa lugha zingine zote na kwa hiyo ndio inayofunzu kuitwa MAME-LUGHA kutokana na hii mame lugha kumezalika lugha zingine nne ambazo ni B C D E.lugha hizi ni dada lugha kwa zozote kwa kuwa zimetokana na mame-lugha kutokana nazo vilevile kumezalika vilugha vingine ambavyo kwa muktdha huu vinajitokeza kama lahaja. Dada lugha zilizo katika ujirani zinakuwa na ukaribu wa kuelewa kimuundo kuliko zile zilizo kwenye masafaya mbali, hivyo basi katika kielelezo hiki mahusiano yaliyopo katika B,C ni ya kali kuliko yale yaliyopo baina yaB C au E

c) KIGEZO CHA UAINISHAJI LUGHA KIUAMILIFU

Kigezo hiki cha uainishaji lugha ujikita katika maswala ya isimu jamii,hivyo basi kigezo cha uainishaji lughakiuamilifu uainisha lugha kwa jinsi zilivyo katika isimu jamii,katika isimu jamii zipo aina mbalimbali za lugha kama ifuatayo

- ❖ Lugha za kwanza
- ❖ Lugha mama
- ❖ Lugha sanifu
- ❖ Lugha ambayo si sanifu
- ❖ Lugha bandia au lugha unde
- ❖ Lugha vipindi au msimu
- ❖ Lugha kutegemea matumizi
- ❖ Lugha za taifa
- ❖ Lugha za kimataifa
- ❖ Lugha rasmi
- ❖ Lugha za pijini na krioli

KIGEZO CHA UAINISHAJI LUGHA KIMUUNDO

Kigezo hiki ujulikana pia kama cha uainishaji lugha kitaipolojia. Hii ni kwa sababu ni muundo wa lugha unaozingatiwa katika kuzitia lugha katika makundi mbalimbali. kigezo hiki ndicho kiaminikacho Zaidi kwa sababu data yake ni ya kuonekana na vilevile haiambatani na maswala ya pembeni kama vile ya kimaeneo. Kigezo hiki ujikita katika muundo wa lugha (fonolojia mofolojia sintaksia leksia semantiki).

Whitely, w.h. (1974). Language in kenya. Nairobi: Kenya

Guthrie, m (1967-71). Comparative bantu . international publishers

Guthrie, m (1948). The classification of the bantu language. London. Oxford university press

Antilla, r. (1972). Introduction to historical and comparative linguistics. London: macmillan.

Habwe, j. na karanja, p. (2004). Misingi ya sarufi ya Kiswahili. Nairobi. Phonix publishers.

Labor, w. (1994). Principles of linguistics change. Oxford.: Blackwell publishers.

Lehman, w. (1992). Historical linguistics. London. Routledge

Homber, j. na hyman, l. (1999). Bantu historical linguistics. Csl publishers.

A

- [Kiaweer](#)

B

- [Kibukusu](#)
- [Kiburji](#)

C

- [Kichonyi](#)
- [Kichuka](#)

D

- [Kidaasanach](#)
- [Kidahalo](#)
- [Kidawida](#)
- [Kidigo](#)
- [Kiduruma](#)

E

- [Kiambu](#)

G

- [Kigiryama](#)
- [Kigujarati](#)
- [Kigusii](#)

I

- [Kiidakho](#)
- [Kiilwana](#)

K

- [Kikabaras](#)
- [Kikalenjin](#)
- [Kikamba](#)
- [Kikeiyo](#)
- [Kikuyu \(lugha\)](#)
- [Kikipsigis](#)
- [Kikuria](#)

L

- [Kilogooli](#)
- [Kiluo \(lugha ya Tanzania\)](#)

M

- [Kimaasai](#)
- [Kimarama](#)
- [Kimarkweeta](#)
- [Kimeru \(Kenya\)](#)
- [Kimolo \(Kenya\)](#)
- [Kimwimbi-Muthambi](#)

N

- [Kinandi](#)
- [Kinyore](#)

O

- [Kiokiek](#)
- [Kiomotik](#)
- [Kiorma](#)
- [Kioromo-Kusini](#)

P

- [Kipokomo](#)
- [Kipokoot](#)

R

- [Kirendille](#)

S

- [Kisaamia](#)
- [Kisabaot](#)
- [Kisagalla](#)
- [Kisamburu](#)
- [Kisomali](#)
- [Kisuba \(Kenya\)](#)
- [Kiswahili](#)

T

- [Kitachoni](#)
- [Kitaveta](#)
- [Kiterik](#)
- [Kiteso](#)
- [Kitharaka](#)
- [Kitugen](#)

- [Kiturkana](#)

W

- [Kiwaata](#)

Y

- [Kiyaaku](#)